



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO



SLP 2324

KILOLO

Tanzania

elephone:0262968010

Fax:0262968010

Website:www.kilolodc.go.tz

Email:ded@kilolodc.go.tz/ded.kilolo@iringa.go.tz

TANGAZO LA KUPATA WAZABUNI WA VIFAA VYA UJENZI ('LOCAL MATERIALS SUPPLIERS)

UJENZI WA SHULE YA WASCHANA WILAYA YA KILOLO , MKOANI IRINGA

TAREHE YA TANGAZO : 04/09/2023

ZABUNI NA ;LGA/027/2022/2023/RSSG/CR/FA/G/01-12

Halmashauri ya wilaya kilolo imepata pesa kwa ajili ya ujenzi wa shule ya waschana ya mkoa, itayojengwa kijiji cha **Mbigili** kata ya **Lugalo**.

Ujenzi huu unategemea kutekelezwa kwa utaratibu wa 'Force Account' .

Aidha, ili kutekeleza mradi kwa utaratibu wa 'Force Account' watekelezaji wanatakiwa kununua vifaa vya ujenzi ambavyo vitatumika na fundi Mkuu kwa majengo yanayotegemewa kujengwa.

Aidha bei ya kifaa husika ni mpaka mzabuni afikishe eneo la mradi unakotekelezwa.

Baadhi ya vifaa vya ujenzi (Materials from Local Suppliers) vinavyohitajika ni kama inavyooneshwa katika jedwari hapa chini.

LOT 1-12

SN	KIFAA	KIPIMO	KIASI KWA M ³ & EA
1	MCHANGA MNENE(mchanga mugumu)	M ³	
2	MCHANGA MWEMBAMBA(plaster works)	M ³	
3	MAWE HARDCORE	M ³	
4	KIFUSI chenye changarawe(MORAM)	M ³	
5	KOKOTO $\frac{3}{4}$ ZILIZOPONDWA KWA MKONO AU MACHINE(LOCALAGGREGATES)	M ³	
6	KOKOTO $\frac{1}{2}$ ZILIZOPONDWA KWA MKONO AU MACHINE(LOCALAGGREGATES)GRANITE AGGREGATES	M ³	
7	TAFALI YA BLOCK inch 6 , (3.5 MPa) MINIMUM COMPREHENSIVE STRENGTH	EA	
	JUMLA		

Hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya , Wilaya ya Kilolo anawatangazia wazabuni wote wenye uwezo, sifa na uzoefu wa kufanya kazi tajwa hapo juu .

Sifa na masharti kwa wazabuni wanaohitajika.

1) Mzabuni lazima awe amesajiliwa kufanya biashara ya bidhaa zilizotajwa katika tangazo hili, na awasilishe nyaraka zifuatazo:

a) Nakala ya Leseni ya Biashara.

b) Cheti cha Namba ya Utambulisho ya Mlipa Kodi (TIN).

c) Cheti cha usajili wa ' BRELA'.

d) Barua inayoonesha kwamba bei ya vifaa vya ujenzi alivyojaza hazitabadirika kwa muda wa miezi sita (06).

e) Barua ya maombi ikitaja vifaa vya ujenzi anazoomba.

f) Wasifu wa kampuni (Company Profile).

g) Kila lot iombwe peke yake na juu ya bahasha onesha unaomba lot ipi.

- 2) Mzabuni atalipwa malipo yake baada ya kuleta vifaa vya ujenzi alivyoshishinda (Post-paid).
- 3) Mzabuni lazima awe na mashine ya ki-eletroniki ya kutolea risiti (EFD Machine) na awasilishe nakala ya uthibitisho wa mashine hiyo.
- 4) Mzabuni lazima awasilishe nakala ya kitambulisho cha benki cha kampuni husika.
- 5) Uchambuzi wa zabuni (Evaluation) utafanyika kulingana bei halisi ya soko kwa kila 'materials' au kifaa kinachohitajika katika mradi, na siyo ujumla wa hati msako (quotation).
- 6) Mzabuni atakayeshinda kuleta 'materials' za ujenzi/vifaa lazima asaini mkataba/makubaliano kabla ya kuleta vifaa vya ujenzi alivyoshinda.
- 7) Mwombaji atatakiwa kudurufu (photocopy) nakala ya hati msako (Quotation) kwa gharama zake mwenyewe ili kujaza, kufunga kwa lakili(sealed) na kuwasilisha nakala halisi (original) moja na nakala vivuli (copies) mbili.
- 8) Inasisitizwa kuwa mzabuni lazima ajaze bei ya vifaa vya ujenzi na kubainisha gharama za usafiri hadi eneo la ujenzi na malipo yatafanyika baada ya vifaa hivyo kupokelewa katika eneo la mradi husika. .
- 9) Maomhi ya zabuni yawasilishwe kwa njia ya mkono ofisi ya
MKURUGENZI MTENDAJI MAKAO MAKUU CHUMBA NA 65

10. Mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni tarehe 11/09/2023 saa 8.00 Mchana na ndiyo siku ya ufunguzi wa zabuni.

Tangazo hili Limetolewa na:

Dr John Mwingira

Kny: Mkurugenzi Mtendaji (W)

Kilolo

Kny: MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KILOLO